HABARI

**Serikali awamu ya sita yavunja rekodi ongezeko la wanyama pori**

Uk.5



**WAZIRI MKUU ASISITIZA KUWA NA UTULIVU NCHINI**

Uk. 4



**SWALA YA TARAWEHE YAPIGWA MARUFUKU DRC**

Uk.5

Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvinews@gmail.com

GAZETI LAKO

JAMVI LA HABARI

ISSN Na 2683 - 6548: Toleo Na. 2541 JUMANNE MACHI 04, 2025 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

# MSAADA WA KISHERIA WA DK. SAMIA WAPONGEZWA KILA KONA NCHINI

- **Wananchi** wampongeza Rais kwa kubuni mpango huu wataka uwe endelevu
- **Waliopata** msaada wakiri sasa serikali yao inajali changamoto zao
- **Maelfu** waliofikiwa wasema lengo limefikiwa kutoa elimu na msaada

Uk.4

**KAMPENI hii ya msaada wa kisheria ya Mama Samia imeanzishwa maalumu kwa lengo la kuweza kuwasaidia wananchi hasa wa hali ya chini kupata msaada wa kisheria kutoka kwa wataalamu mbali mbali kutoka Halmashauri pamoja na baadhi ya mawakiri kutoka Wizara ya Katiba na sheria na kwamba msaada huo unatolewa bila malipo yoyote lengo ikiwa ni kuwasaidia wananchi, amesema Wakili George.**



## Dk. Mpango akemea unyanyasaji wa kijinsia

Uk.3



# MSAADA WA KISHERIA WA DK. SAMIA WAPONGEZWA KILA KONA NCHINI

NA MWANDISHI WETU

MUITIKIO wa hali ya juu umejitokeza maeneo mbalimbali nchini wakati wa muendelezo wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia, ambapo Watanzania wengi wamefikiwa na kupongeza mpango huo wanaoutaja kama ndiyo mkombozi wa wanyonge.

T ambapo wananchi wengi hasa wa kipato cha chini, wanafunzi, wajane na wahanga wengine wameonekana kurudishiwa matumaini ya kupata haki zao kutoka katika masuala mbalimbali.

Miungoni mwa mambo wanayotakiwa wahanga wanaokutana na wanasheria kwa ajili ya kupata msaada huo ni kutoa maelezo sahihi.

Hivi karibuni akiwa Jijini Arusha Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini, aliwasisitiza wananchi kutoa maelezo sahihi kwa watoa huduma za msaada wa kisheria ili kufanikisha kutatua changamoto zinazowakabili.

Aliyataja maeneo yanayokumbwa na migogoro zaidi ni pamoja na ardhi, mirathi, ndoa na masuala mengine ya kisheria ambayo yanapata ufumbuzi.

Alitoa rai hiyo wakati alipotembelea banda la Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na mabanda mengine kuelekea wiki ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambayo itafanyika Machi 8 mwaka huu mkoani Arusha.

Ukiacha maeneo mbalimbali ya nchi yaliyofikiwa na Kampeni hiyo, Wilayani Bagamoyo katika mkoa wa Pwani jumla ya wananchi elfu 14 kutoka kata nane zilizopo katika Halmashauri hiyo kutoka katika makundi mbali mbali waliokuwa wakikabiliwa na changamoto mbali mbali kama ndoa, mirathi, migogoro ya ardhi, pamoja na ukatili wa kijinsia wamefikiwa na kampeni hiyo ya msaada wa kisheria.

Wakiri George Molel ambaye ni mratibu wa huduma ya kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia katika Halmashauri ya Bagamoyo alisema kwamba lengo kubwa la msaada huo wa kisheria ni kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi ambayo itawasaidia kujua haki zao za msingi katika masuala mbali mbali.

Wakiri George amebainisha kwamba katika kampeni hiyo ya msaada wa kisheria Katika Halmashauri ya Bagamoyo imeweza kufanikiwa kupitika katika kata nane, zikiwemo Fukayose,Makurunge, Yombo, Kiromo,Kerege, Nianjema, Kisutu, pamoja na Kata ya Dunda ambapo wameweza kutoa elimu kwa wanafunzi, walimu, wananchi wa kawaida, makanishani pamoja na makundi mbali mbali.

ìKampeni hii ya msaada wa kisheria ya Mama Samia imeanzishwa maalumu kwa lengo la kuweza kuwasaidia wananchi hasa wa hali ya chini kupata msaada wa kisheria kutoka kwa wataalamu mbali mbali kutoka Halmashauri pamoja na baadhi ya mawakiri kutoka Wizara ya Katiba na sheria na kwamba msaada huo unatolewa bila malipo yoyote lengo ikiwa ni kuwasaidia wananchi,îamesema Wakiri George.

Kwa upande wake Afisa maendeleo ya Jamii Kata ya Kerege Lilian Mkosyange amesema kuwepo kwa changamoto mbali mbali kwa wananchi ikiwemo suala la wakinababa kuwa na tabia ya kutelekeza familia zao na kupelekea mama na watoto kubaki peke yao bila msaada wowote.

Naye mmoja wakazi wa Wilaya ya Bagamoyo Samweli Ringo amempongeza kwa dhati Rais wa awamu ya sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuanzisha kampeni hiyo na kubainisha kwamba elimu ambayo wameipata itakwenda kuwa mkombozi mkubwa kwani wameweza kujifunza mambo mbali mbali juu ya msaada wa kisheria.

Kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia inaendelea kufanyika katika Mkoa wa Pwani ambapo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo tayari imeshapita katika kata zipatazo nane na kutoa msaada wa kisheria katika masuala ya Ndoa, mirathi,migogoro ya ardhi, wosia,matunzo ya watoto,kesi za madai,unyanyasaji wa kijinsia, pamoja na haki za binadamu na mambo mengine ya kimsingi yanayohitaji msaada huo.



# SWALA YA TARAWEHE YAPIGWA MARUFUKU DRC

NA MWANDISHI WETU

BARAZA kuu la Waislamu katika Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) Limetoa Taarifa ya kusitishwa kwa Swala ya Taraweh Misikitini katika Miji ya mashariki nchini humo Goma,Bukavu, Uvira, Baraka na miji mingineyo kwa sababu ya hali ya usalama hairuhusu kutoka nje nyakati za usiku

Baraza hilo limewataka waislamu wote maeneo hayo kuchanganya swala ya magharib na Swala ya Isha na kurejea majumbani kabla ya Giza kuingia.

Hatua hiyo imekuja kufuatia mashambulizi ya M23 ma majeshi ya Serikali ya DRC yalikuja kwa nguvu na kutishia ukanda huo, huku mateso, mauaji pamoja na vitisho vya milio ya silaha nzito zilizosambaa kila kona na kuzua hofu kwa wananchi wa nchi ya Kongo pamoja na ndugu na jamaa wa nchi mbalimbali waliokuwa na ndugu zao huko.

## ERIKALI AWAMU YA SITA YAVUNJA REKODI ONGEZEKO LA WANYAMA PORI

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana amesema ongezeko la idadi ya Wanyamapori katika hifadhi za Wanyama hapa nchini imetokana na juhudi za serikali kushirikisha wadau wa uhifadhi wa Wanyamapori na wananchi kwa ujumla hali iliyopelekea kukua kwa utalii na uchumi katika Taifa.

Ameyasema hayo jana jijini Dodoma katika maadhimisho ya 11 ya Siku ya Wanyamapori Duniani ambapo amesisitiza Tanzania inaongoza Duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya wanyama aina ya Simba, Chui, Nyati na ni ya tatu kwa idadi wa Tembo Duniani huku akifafanua kuwa mafanikio hayo ni kutokana na kuitangaza vyema sera ya Utalii ndani na nje ya nchi na kuboresha jeshi la uhifadhi.

ìWanyamapori ni rasilimali muhimu katika uchumi wa nchi yetu kupitia utalii ambao unachangia zaidi ya asilimia 25 ya fedha za kigeni, asilimia 17.1 ya Pato la Taifa na ajira takribani milioni 1.6 zilizo rasmi na zisizo rasmi, hadi Mwaka 2024, Sekta ya Utalii imevunja rekodi kwa kufikia jumla ya watalii 5,360,247 na watalii wa Kimataifa imefikia 2,141,895 huku watalii wa ndani wakiwa 3,218,352. Kutokana na mapato ya utalii imefikia Dola za Marekani Bilioni 3.9î amesema Waziri Chana

Aidha, ameweka bayana kuwa juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan za kutangaza utalii kwa vitendo ndani na nje ya nchi kupitia Programu ya Tanzania the Royal Tour na Amazing Tanzania imesaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza hamasa kwa watalii wa ndani na nje ya nchi kutembelea hifadhi za utalii na Wanyamapori hapa nchini.

Katika hatua nyingine, Waziri Dk. Chana amesema Serikali kupitia Wizara Hiyo imeendelea kushirikiana na wadau wa uhifadhi kuchukua jitihada za makusudi ikiwemo kulinda na kuendeleza uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori, kudhibiti ujangili wa nyara na kitoweo na uhifadhi endelevu wa mapito ya wanyamapori ili kuimarisha mifumo ikolojia ya uhifadhi sambamba na ushirikishwaji wa jamii kupitia maeneo ya Jumiya za Hifadhi za Wanyamapori.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo anayeshughulikia Maliasili, CP. Benedict Wakulyamba amesema Wizara itaendelea na mikakati ya kutunza na kuhifadhi Wanyamapori kwa kuweka mazingira wezeshi na kutangaza sera ya Utalii nje ya nchi kwa kukaribisha wawekezaji, kuboresha maeneo ya hifadhi, kuboresha maisha kwa watumishi wa wahifadhi na vitendea kazi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

# MAKONDA ATOA ONYO WANAOPANDISHA BEI ZA VYAKULA

NA MWANDISHI WETU

MKUU wa Mkoa wa Arusha Mhe. Paul Christian Makonda ameonya wafanyabiashara wa Mkoa wa Arusha kujiepusha na upandishaji wa Gharama za vyakula vinavyotumika zaidi wakati huu wa msimu wa mfungo wa Mwezi mtukufu wa Ramadhan, akitangaza kuja na Operesheni maalum ya kutembelea maduka ili kubaini wafanyabiashara wanaotumia mfungo wa Ramadhan kujitafutia faida ya ziada.

Niwasihi, mwezi huu ( Mwezi mtukufu wa Ramadhan) sio mwezi wa kutengeneza faida, mwezi huu ni wa kutafuta baraka, faida unayoitafuta inaweza kuna kukugharimu sana, ukajikuta umepata magonjwa yakala mpaka na mtaji wako. Wenzako wanapofunga kwaajili ya kumuomba Mwenyenzi Mungu, jitahidi na wewe uwe sehemu ya baraka ya kuhakikisha kuwa huwapi vikwazo.î Amesema Mhe. Makonda.

Mhe. Makonda pia kando ya kuarifu kuwa Mkoa unaandaa futari kwaajili ya wananchi wa Mkoa wa Arusha, amewatakia Kheri pia Waislamu wa Mkoa wa Arusha kwenye mfungo waliouanza mwishoni mwa Juma lililopita sambamba na kwa Wakristo ambao wanatarajiwa kuanza mfungo wa Kwaresma hivi karibuni, akiomba kuwa funga zao zikafanyike kuwa baraka na kichocheo cha amani na Upendo katika Mkoa wa Arusha.



# BIL 233.7 ZATUMIKA MABORESHO YA VETA




NA MWANDISHI WETU

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufunzi Stadi (VETA), Anthony Kasore amesema serikali kwa mwaka 2021/2024 ilitenga kiasi cha Sh. 233.7 bilioni kwa ajili ya kufanya maboresho na ujenzi wa miundombinu ya VETA hapa nchini. Anaripoti Apaikunda Mosha. Dodoma Ö (endelea).

Hayo ameyasema jana, wakati anatoa taarifa kwa vyombo vya habari juu ya mweleko wa utekelezaji wa majukumu na mafanikio ya mamlaka ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa mwaka 2021/24.

Kasore amesema, tangu uanzishwaji wake mwaka 1994 VETA ilipewa majukumu ya kuhakikisha kwamba inasimamia, kugharamia na kuratibu ufunzaji wa elimu ya ufundi stadi nchini, ili kuwe na mafundi mahiri wakutosha katika kutekeleza majukumu ya shughuli mbalimbali zinazohitaji rasilimali watu wenye ujuzi.

Akiainisha miradi mbalimbaliya maendeleo iliyofanywa na inayoendelea kufanywa amezungumzia kukamilika kwa ujenzi wa vyuo 33 katika wilaya 29 na mikoa minne, uliogharimu takribani bilioni 94.5, sambamba na hilo serikali imeendelea kuhakikisha ujenzi wa vyuo 64 unaendelea katika maeneo mbalimbali na tayari imetoa bilioni 103 kwa mradi huo.

Ameeleza pia, maboresho ambayo serikali imefanya katika vyuo vya VETA amesema kiasi takribani biloni 14.2 imetolewa kwa ajili ya maboresho katika vyuo ndani ya wilaya mbalimbali, na kwenye manunuzi ya vifaa vyenye ubora na vinavyokidhi mahitaji kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, takribani bilioni 22 zimetolewa ili waweze kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

Aidha maboresho mengine ni kwenye uboreshaji wa mitaala 42, pamoja na kutengeneza mingine mipya 20 ambayo inajumuisha TEHAMA, michezo, umeme, magari, mitambo, kilimo, ukarimu, usafirishaji, biashara, mavazi, madini na urembo ili wawe na uwezo wa kujitengenezea kipato na kuliingizia taifa kipato.

Ameeleza pia katika vyuo vya kurekebisha tabia (magereza) jumla ya watu 214 katika vituo vya Ukonga, Arusha na Morogoro wameweza kufanyiwa tathmini ya ujuzi wao, na wamepatiwa vyeti ili waweze kuaminika nakufanya kazi ya kuridhisha.

Aidha katika program ya urasimishaji ujuzi ya Rais Samia amesema mpaka sasa wameshafanya urasimishaji wa watu 1600 na mpaka ifikapo juni 2026 wanatarajia kuwafikia zaidi ya wananchi 80,000 ili kuhakikisha uwa watu wanatambulika na wanapata zabuni mbalimbali.

Kasore ameeleza namna ya upatikanaji wa mafunzo kutokana na teknolojia muhitaji hatafika chuoni amesema, unaweza kusoma katika mifumo kama mfumo wa visomo mpaka atakapohitajiwa kufika chuoni kusoma kwa vitendo, mafunzo kwa masafa pamoja Akili unde (Artificial Intelligence).

Sambamba na hayo amesema matarajio ya VETA ni kutoa tunuku za kimatafa ili kumuhakikishia mtu kupata kupata fursa za ajira maeneo mengi, amesema kutakuwa na vyuo vya kimataifa 14 ambavyo vitatoa mafunzo hayo na viwili kati ya hivo tayari vimeeanza kazi ya utoaji wa elimu ya uungaji wa vyuma.

# DK. MPANGO AKEMEA UNYANYASAJI WA KIJINSIA

NA MWANDISHI WETU

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ametoa wito kwa Watanzania kukemea vitendo vya ukatili ulioshamiri dhidi ya wanawake na watoto na kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya wahusika.

Dkt. Philip Mpango alitoa wito huo wakati wa Kongamano la Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Kanda ya Magharibi lililofanyika katika Ukumbi wa NSSF mkoani Kigoma.

Ametaja baadhi ya vitendo hivyo kama mauaji, ubakaji, ulawiti, kupigwa, kunyanyaswa, kunyimwa haki za kumiliki ardhi na mali nyingine za familia, urithi, fursa za elimu, ukeketaji, adhabu kubwa zisizowiana na kosa alilotenda mtoto.

Makamu wa Rais amesema baadhi ya vitendo hivyo vinafanywa na wanafamilia au ndugu wa karibu na sehemu kubwa ya vitendo hivyo havitolewi taarifa kwenye vyombo vya sheria ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Ameongeza kwamba wakati mwingine, baadhi ya mila na desturi katika jamii hutumika kuwakandamiza wanawake na watoto.




Aidha Makamu wa Rais ametoa rai kwa Kongamano hilo ambalo idadi kubwa ya washiriki wake ni wanawake na ambao ni walezi wa familia, kuelekeza nguvu pia katika kumlinda mtoto wa kiume ili kumhakikishia usalama wake. Amesema uwekezaji jitihada kidogo kwa mtoto wa kiume imepelekea mtoto wa kiume kujikuta katikati ya matatizo lukuki yakiwemo matumizi ya madawa ya kulevya, ushoga na aina nyingine za ukatili.

Makamu wa Rais ili kuendelea kuongeza mchango na ushiriki wa Wanawake katika utunzaji wa mazingira na kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia, hakuna budi kongamano hilo kujadili na kuibua mikakati madhubuti na yenye kutekelezeka ili kufikia malengo hayo.

Amesisitiza umuhimu wa kuimarisha utoaji wa elimu na hamasa kwa umma kuhusu utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati safi ya kupikia. Amesema elimu kwa umma na hamasa ni muhimu katika utunzaji endelevu wa mazingira kwa kuwa tabiawatu ndiyo kisababishi kikuu cha uharibifu wa mazingira.

Makamu wa Rais ametoa rai kwa taasisi kama Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), TEMDO na nyingine kutafiti na kutengeneza teknolojia mbalimbali zinazotumia nishati safi na zenye gharama nafuu ili ziweze kusaidia uhamaji kwenda kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia. Aidha ametoa wito kwa wafanyabiashara wakubwa na sekta binafsi kwa ujumla kujitolea kusaidia majiko na teknolojia rahisi kwa shule na vituo vinavyolea watoto na watu wenye mahitaji maalum.

Makamu wa Rais amesema Serikali ya Awamu ya Sita inatekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 ñ 2034 ambao unalenga kuhakikisha 80% ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Vilevile amesema Serikali imesaini makubaliano ya awali na wawekezaji kuhusu Ruzuku ya Sh. Bilioni 8.64 kwa ajili ya nishati safi ya kupikia, ambapo jumla ya majiko 452,455 yamepata ruzuku kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia kwa wananchi kwa gharama nafuu.

Hali kadhalika Makamu wa Rais amewasihi wanawake kushiriki kikamilifu katika kutoa hamasa kuhusu jukumu muhimu la kujiandikisha kupiga kura, kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na kushiriki kuchagua viongozi wanaowapenda. Amesema ni jukumu la kila mmoja kujenga na kudumisha umoja, amani, mshikamano na kuepuka vurugu katika mchakato wote wa uchaguzi.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Mhe. Mwanaidi Ali Khamis amesema dhima ya kongamano hilo ni kuhimiza wanawake na jamii kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati safi. Amesema pia Kongamano limedhamiria kuhamasisha wanawake kukaa na familia pamoja na kupata muda mzuri zaidi ili kujenga malezi na makuzi kwa mustakbali wa familia bora.

Kongamano la wanawake kanda ya magharibi ni sehemu ya maadhimisho ya Siku Kimataifa ya Wanawake Duniani ambayo kilele chake kitakuwa tarehe 8 Machi, 2025 Jijini Arusha. Kongamano hilo lina kaulimbiu isemayo ëMchango na ushiriki wa Wanawake katika matumizi ya nishati safi na utunzaji wa mazingiraí.

# MALEFU YA WANAFUNZI WAFIKIWA MSAADA WA KISHERIA WA DK SAMIA

NA MWANDISHI WETU

WANAFUNZI zaidi ya elfu 2423 wa shule za msingi na sekondari zilizopo Kata ya Tumbi katika Halmashauri ya Kibaha mji mkoani Pwani wamenufainika na kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Simia kwa kuweza kujengewa uwezo wa masuala mbali mbali yanayohusiana na haki zao za msingi ikiwemo suala zima la unyanyasaji wa kijinsia, kuepukana na kufanya vitendo vya mapenzi wakiwa shuleni ili kuepukaana kabisa na wimbi la mimba za ututoni.

Akizungumza na baadhi ya wanafunzi kuhusiana na kampeni hiyo Wakili George Banoba kutoka Wizara ya Katiba na sheria amesema kwamba wamefanikiwa kupita katika shule mbali mbali zikiwemo shule za msingi tatu pamoja na shule ya sekondari Mwanalugali kwa lengo la kuweza kutoa elimu ya masuala mbali mbali yanayohusiana na sheria. Banoba amebainisha kwamba katika kampeni hiyo wameweza kuambatana na wadau mbali mbali wa sheria akiwemo pamoja na Afisa ustawi wa jamii pamoja na mkuu wa Dawati lajinsia Wilaya ya Kibaha kwa lengo la kuweza kupata elimu kwa wanafunzi na kuwaajengea uwezo juu ya kutambua haki zao za msingi ikiwemo mambo ya unyanyasaji wa kijinsia. ìTumeanza rasmi kampeni yetu ya msaada wa kisheria ambapo tumeanza katika kata ya Tumbi na tumefanikiwa kuwafikia wanafunzi zaidi ya 2400 na wameweza kufundishwa masuala mbali mbali ya msaada wa kisheria bure na kwamba katika Halmashauri ya mji Kibaha watakwenda katika kata zipatazo 10 ambapo watatoa msaada wa kisheria katika maeneo ya migogoro ya ardhi, ndoa, miradhi, pamoja na usaidizi mwingine unaohusina na mambo ya kisheria,îamesema



Kwa upande wake Kaimu mkuu wa shule ya sekondari Mwanalugali Jeriko Rogers na pamoja na mwanafunzi wa shule hiyo Mwasalobo Komalumo wamempongeza Rais wa wawamu ya sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuanzisha kampeni ambayo itaweza kuwa ni mkombozi mkubwa katika kuwasaidia katika suala zima la msaada wa kisheria.

Naye Mkuu wa wa dawati la Kjinsia na watoto Wilaya ya Kibaha pamoja na Afisa ustawi wa jamii katika Halmashauri ya Kibaha mji wamebainisha kwamba kampeni hiyo itakwenda kuwa mkombozi na msaada mkubwa katika kuwasaidia wanafunzi pamoja na wananchi wengine kuweza kupata haki zao za msingi.

Kampeni ya msaada wa kisheria wa Mama Samia inaendelea kufanyika katika Mkoa wa Pwani ambapo itapita katika Halmashauri zote tisa kwa lengo la kuweza kutoa elimu ya masuala mbali mbali ikiwemo mambo ya migogoro ya ardhi, ndoa, mirathi pamoja na mambo mengine ya msingi yanayohitaji msaada wa kisheria.


# TANGAZA NASI SASA

*Unatamani kukuza biashara yako kutoka hapo ilipo kuwa kubwa na yenye mantiki zaidi?*

- *Unatamani kuongeza kipato, uelewa na upana wa shughuli zako za kila siku?*
- *Je unataka kuwafikia wateja wako ndani na nje ya nchi kwa kiasi kikubwa ili kukuza biashara na huduma yako?*
- *Fahamu kwamba JAMVI LA HABARI na mitandao yake ya kijamii kama Youtube, Instagram, Facebook, Website na Twitter hutembelewa na maelfu ya wasomaji kila siku Duniani kote.*
- *Hivi unafahamu kuwa JAMVILAHABARI kwa sasa ni moja kati ya Media chache zinazo ongoza kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazotokea nchini na Duniani kwa ujumla?*

*TANGAZA SASA NA JAMVI LA HABARI KWA PUNGUZO KUBWA LA BEI UPATE MATOKEO YA HARAKA.*

*Kwa matangazo yote kama vile minada, kupotelewa kwa vyeti vya shule, matangazo ya makampuni, nafasi za kazi, zabuni za kazi, maonyesho, dawa za asili, taasisi za elimu, taasisi za dini na mengine mbalimbali mbali mbali.*

*Ni rahisi sana, wasiliana nasi kupitia Whatsap namba +255659555744 au tupigie katika +255743777778 au +255659555744 GHARAMA ZETU NISAWA NA BUREE JAMVILAHABARI; TUMECHAGUA KUKUHUDUMIA www.jamvilahabari.co.tz*

# WAZIRI MKUU ASISITIZA KUWA NA UTULIVU NCHINI

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa ametoa wito kwa viongozi wa dini waendelea kuliombea Taifa na viongozi wake kwani pasipo na amani na utulivu nchi haiwezi kutimiza malengo ya kuwaletea Watanzania maendeleo ya kiuchumi.

ìNchi haiwezi kuwa na uhuru wa kuabudu, pasipo amani hatuwezi kufanya shughuli za uzalishaji mali. Katika eneo hili ninawapongeza na kuwashukuru madhehebu yote ya dini kwa kuendelea kuiombea nchi yetu amani, mshikamano na utulivu.î

Waziri Mkuu ametoa wito huo jana usiku (Februari 28, 2025) katika viwanja vya Leaders Club alipomuwakilisha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati maombi maalum ya Kitaifa iliyoandaliwa na Umoja wa Viongozi wa Makanisa.

Alisema suala la ushirikiano kati ya Serikali na madhehebu ya dini, limekuwa kipaumbele cha Serikali ya awamu ya sita na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia amekuwa kinara katika hilo.

ìAmekuwa akiwashirikisha viongozi wa dini katika masuala mbalimbali, wakati mwingine amefanya nao mazungumzo na anawatembelea. Vitendo hivyo vinadhihirisha jinsi Serikali inavyowathamini viongozi wa madhehebu ya dini.î

Katika ibada hiyo viongozi hao wa Makanisa walitumia fursa hiyo pamoja na mambo mengine kuliombea Taifa lidumishe muungano, amani, utulivu, umoja na mshikamano, pia waliuombea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Alisema kuwa Serikali kwa upande wake imekuwa ikichukua hatua za makusudi za kuinua ustawi wa wananchi wote bila kujali itikadi zao za imani, hizo ni pamoja na utekelezaji wa mipango na mikakati kuhakikisha kuwa wananchi wote wanafikiwa na huduma bora mbalimbali za kijamii.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza alipomwakilisha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Maombi Maalum ya Kuliombea Taifa yaliyoandaliwa na Umoja wa Viongozi wa Makanisa nchini kwenye Viwanja vya Leaders Club jijini Dar es Salaam.

Hivi karibuni Waziri Mkuu alisisitiza nchi kuwa na amani alipokuwa

alipokuwa mgeni rasmi katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM uliofanyika katika Uwanja wa Nguzo Nane, Mjini Maswa na kuhudhuriwa na umati wa wanachama wa chama hicho pamoja na wananchi kwa jumla.



Akizungumza katika mkutano huo Mh. Majaliwa aliwashukuru Wana Maswa kutokana na idadi kubwa ya wananchi waliojitikeza wakiwemo wana CCM na wapenzi wa chama hicho na kusisitiza kuwa wingi wao unatokana na kuridhishwa na utekelezaji wa Ilani ya chama hicho.

“Unaweza ukakaa mjini hapa usijuwehaoa kuna nini, lakini ukipita hapa utajua kuwa Chama Cha Mapinduzi leo na serikali yake leo kipo hapa” alisema.

Mh. Majaliwa alisema miungoni mwa mambo ambayo Serikali ya CCM imefanikisha ni katika Sejta ya Elimu ambapo utelekezaji wa uejenzi wa Shule za Msingi, Sekondri Vyumba vya madarasa na mengine ya aina hiyo yamefanyika na kazi bado inaendelea.

Kuhusu Sekta ya Maji Mhe majaliwa alisema, Serikali inayoongozwa na CCM imejipanga kuhakikisha wananchi wanapata maji siyo kwa kuyafuata mbali bali hadi yatakapoweza kuingia ndani ya nyumba za wananchi, hayo ndiyo malengo ya serikali.

Alisema tayari miradi mikubwa imeanza na mingine inaendelea kukamilisha ili kuondoa shida ya maji kwa wananchi koite Tanzania, alitoa mfano wa kazi za uchimbaji visima katika maeneo yaliyokuwa na maji mengi pia utoaji maji katika maziwa makubwa kazi ambayo inafanyika kwa kutumia Teknolojia ya kisasa itaweza kuondoa shida ya maji hapa nchini.

Mh Majaliwa pia amezungumza serikali ya CCM kuwa itahakikisha inatatua changamoto mbalimbali ikiwezmo upatikanaji wa umeme kila sehemu ili wananchi wapate huduma hiyo.

Kuhusu sekta ya afya alisema Serikali imejipanga kupunguza gharama za matibabu kwa kujenga hospitali kubwa na kuboresha vituo vya afya na Zahanati afya kazi ambayo imeanza kwa kasi na pia itaendelea ikiwa ni malengo ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan anayetaka kuona Watanzania wanapata huduma bora za afya.

Mwisho wake Waziri Mkuu aliwataka wananchi kudumisha amani kama ndiyo tunu ya utuivu wa Taifa la Tanzania.

# TAHARIRI

## Nida iondoe usumbufu Ugawaji wa vitambulisho

KWA siku za hivi karibuni vituo vya NIDA katika miji na mikoa mbalimbali vimekuwa vikishuhudiwa msongamano mkubwa wa wananchi wanaoshinda hapo kuanzia asubuhi mpaka majira ya jioni, ofisi zinapofungwa.

Wanachofuata katika ofisi hizo ni utekelezaji wa agizo la Mamlaka ya hiyo iliyowataka wananchi wafuatilie vitambulsho vyao, vinginevyo watasitisha matumikzi ya namba.

Kinachoonekana ni kutokuwa na maandalizi ya uhakika kwani idadi kubwa ya wananchi wanapofika katika ofisi hizo, wamekuwa wakikumbana na usumbufu kutoka kwa walinzi na hata mzunguko unaotakiwa kuufuata kabla ya kuelekezwa namna ya kupata kitambulisho.

Sisi tunaona kuwa njia ile ya awali ya kupeleka vitambulisho katika ofisi za Serikali za Mitaa ilikuwa muafakja lakini ilikikosa uratiubu mzuri.

Katika maeneo mengi ya serikali za mitaa tulikuwa tukishuhudia maelekezo ya uwepo wa vitambulisho vya wananchi lakini walipokuwa wakivifuata hata kama maelekezo yanaonyesha vilikuwepo ofisi husika lakini havikuwepo.

Wananchi wengi walijikuta wakitembea kila kata kutafuta vitambulisho vyao bila kupatikana jambo ambalo liliwakatisha tamaa wengi na kukuta vitambulisho vilivyostahili kuwa huku vimepelekwa kule.

Sisi tunadhani njia ya kurudisha zoezi hilo katika ofisi kuu za NIDA ni nzuri, lakini lingeratibiwa vizuri na kuondoa urasimu ili zoezi liende sawia.


Aidha kurudisha maeneo ya aina hiyo kwa namna moja au nyingine itachochea kutokea vitendo vya kuomba rushwa kwa vile wananchi wengi hawapendi kupoteza muda katika jambo wanaloweza kulifanya kwa kutoa rushwa.

Tunadhani itakuwa ni wakati mzuri kwa Mamlaka, kuliangalia tena zoezi hili na kisha kuamua kufanya mawili, au kuboresha ofisi za Serikali za Mitaa na kata au kuweka mazingira mazuri katika ofisi kuu za NIDA.


## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu - 0762 178 678
Idara Ya Matangazo/Masoko - 0743 777 778,
- 0659 555 744
Idara Ya Usambazaji - 0676807684,
- 0787 288 160

Gazeti hili hutolewa na **JAMVI MEDIA GROUP**
S. L. P 78862, Dar es Salaam
**Tel:** +255 676 807684, 255 743 777778
**Email:** jamvinews@gmail.com
www.jamvilahabari.co.tz

*Rais wa Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Cyril Ramaphosa akizungumza jambo na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel John Nchimbi, walipokutana Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Hosea Kutako, Windhoek, nchini Namibia, baada ya mazishi ya Rais wa Kwanza wa Namibia na Baba wa Taifa hilo, Dk. Sam Shafiishuna Nujoma, mwishoni mwa wiki.*

## UCHAMBUZI

# Serikali yasisitiza nidhamu miko ya halmashauri

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ametoa onyo kwa wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi endapo itabainika kuwa vikundi hewa katika maeneo yao vilivyonufaika kupitia mikopo ya asilimia 10, watawajibishwa.

Waziri Mchengerwa ametoa onyo hilo jijini Dodoma wakati wa hafla ya utiaji saini mikataba ya utoaji mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulamavu kati ya halmashauri 10 na benki mitatu.

Amewataka Mkuu wa Mkoa , Wilaya na Wakurugenzi wafuatilie kwakuwa hataki kusikia vikundi hewa. "Nawambia wazi kabisa, tumefika hapa kwasababu kuna watumishi wasio waaminifu ambao walitafuna fedha hizi kwa kukopeshana wenyewe na hawakuwa na sifa ya kupokea mikopo hii."amesema Mchengerwa

Aidha Mchengerwa amesisitiza kuwa uadilifu kwenye fedha hizo na kuwataka wafuatilie vikundi vyote na kuvijua na asisikie vikundi hewa.

"Fedha hizi ni za moto wajibu wetu ni kumsaidia Rais fedha hizi zisiende kuchezewa, naelekeza kikundi hewa kitakachobainika eneo lolote viongozi wa eneo hilo mtapaswa kuwajibika, tumieni vyombo mnavyosimamia kwenye mikoa na wilaya kuhakikisha hakuna vikundi hewa, fedha zisimamiwe na kurejeshwa."amesisitiza

Hata hivyo amesema vikundi vyote vinavyopokea mikopo hiyo vinatakiwa kufanya shughuli za uzalishaji na kurejesha fedha kulingana na mipango ya marejesho.

"Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi tumekubaliana jukumu la usimamizi wa fedha hizi ni la kila mmoja wet una wakati tunamshauri Rais sisi Wizara tulimhakikishia kuanzia kwangu kwamba iwapo kutakuwa na kulegalega kukote mimi na wasaidizi wangu tutalazimika kuwajibika."

Amesema Benki ya NMB itafanya kazi kwenye halmashauri za wilaya za Bumbuli, Itilima, Newala, Manispaa ya Songea, Jiji la Dodoma huku benki ya CRDB itafanya kazi Wilaya za Nkasi, Mji wa Mbulu, Manispaa ya Kigoma na Jiji la Dar es salaam.

Hata hivyo, amesema Benki ya Biashara ya Uchumi itafanya kazi Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

"Zaidi ya Sh.Bilioni 234 zinakusudiwa kupelekwa kwa wananchi kwa njia mbili za utoaji mikopo hiyo ambazo ni kupitia Benki kwa Halmashauri 10 na mikopo iliyoboreshwa kwenye Halmashauri 174.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Tamisemi, Profesa Adolf Ndunguru amesema kuwa kusainiwa mikataba hiyo ni mwanzo wa mapinduzi ya kuhakikisha mikopo hiyo ya asilimia 10 inakuwa na tija tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

# Waziri Mkuu asisitiza k

NA MWANDISHI WETU



WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa ametoa wito kwa viongozi wa dini waendelea kuliombea Taifa na viongozi wake kwani pasipo na amani na utulivu nchi haiwezi kutimiza malengo ya kuwaletea Watanzania maendeleo ya kiuchumi.

ìNchi haiwezi kuwa na uhuru wa kuabudu, pasipo amani hatuwezi kufanya shughuli za uzalishaji mali. Katika eneo hili ninawapongeza na kuwashukuru madhehebu yote ya dini kwa kuendelea kuiombea nchi yetu amani, mshikamano na utulivu.î

Waziri Mkuu ametoa wito huo jana usiku (Februari 28, 2025) katika viwanja vya Leaders Club alipomuwakilisha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati maombi maalum ya Kitaifa iliyoandaliwa na Umoja wa Viongozi wa Makanisa.

Alisema suala la ushirikiano kati ya Serikali na madhehebu ya dini, limekuwa kipaumbele cha Serikali ya awamu ya sita na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia amekuwa kinara katika hilo.

ìAmekuwa akiwashirikisha viongozi wa dini katika masuala mbalimbali, wakati mwingine amefanya nao mazungumzo na anawatembelea. Vitendo hivyo vinadhihirisha jinsi Serikali inavyowathamini viongozi wa madhehebu ya dini.î

Katika ibada hiyo viongozi hao wa Makanisa walitumia fursa hiyo pamoja na mambo mengine kuliombea Taifa lidumishe muungano, amani, utulivu, umoja na mshikamano, pia waliuombea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Alisema kuwa Serikali kwa upande wake imekuwa ikichukua hatua za makusudi za kuinua ustawi wa wananchi wote bila kujali itikadi zao za imani, hizo ni pamoja na utekelezaji wa mipango na mikakati kuhakikisha kuwa wananchi wote wanafikiwa na huduma bora mbalimbali za kijamii.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza alipomwakilisha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Maombi Maalum ya Kuliombea Taifa yaliyoandaliwa na Umoja wa Viongozi wa Makanisa nchini kwenye Viwanja vya Leaders Club jijini Dar es Salaam.

Hivi karibuni Waziri Mkuu alisisitiza nchi kuwa na amani alipokuwa

alipokuwa mgeni rasmi katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM uliofanyika katika Uwanja wa Nguzo Nane, Mjini Maswa na kuhudhuriwa na umati wa wanachama wa chama hicho pamoja na wananchi kwa jumla.

Akizungumza katika mkutano huo Mh. Majaliwa aliwashukuru Wana Maswa kutokana na idadi kubwa ya wananchi waliojitikeza wakiwemo wana CCM na wapenzi wa chama hicho na kusisitiza kuwa wingi wao unatokana na kuridhishwa na utekelezaji wa Ilani ya chama hicho.

“Unaweza ukakaa mjini hapa usijuwehaoa kuna nini, lakini ukipita hapa utajua kuwa Chama Cha Mapinduzi leo na serikali yake leo kipo hapa” alisema.

Mh. Majaliwa alisem
miungoni mwa mamb
ambayo Serikali ya CC
imefanikisha ni kati
Sejta ya Elimu ambap
utelekezaji wa uejenzi w
Shule za Msingi, Sekon
Vyumba vya madarasa
mengine ya aina hiyo y
mefanyika na kazi bad
inaendelea.

Kuhusu Sekta ya M
Mhe majaliwa alisem
Serikali inayoongozw
na CCM imejipanga k

# kuwa na utulivu nchini



> Majaliwa pia amezungumza serikali ya CCM kuwa itahakikisha inatatua changamoto mbalimbali ikiwezmo upatikanaji wa umeme kila sehemu.

na
bo
M
ka
bo
va
dri
na
va-
do

aji
na,
va
u-

hakikisha wananchi wanapata maji siyo kwa kuyafuata mbali bali hadi yatakapoweza kuingia ndani ya nyumba za wananchi, hayo ndiyo malengo ya serikali.

Alisema tayari miradi mikubwa imeanza na mingine inaendelea kukamilisha ili kuondoa shida ya maji kwa wananchi koite Tanzania, alitoa mfano wa kazi za uchimbaji visima katika maeneo yaliyokuwa na maji mengi pia utoaji maji katika maziwa makubwa kazi ambayo inafanyika kwa kutumia Teknolojia ya kisasa itaweza kuondoa shida ya maji hapa nchini.

Mh Majaliwa pia amezungumza serikali ya CCM kuwa itahakikisha inatatua changamoto mbalimbali ikiwezmo upatikanaji wa umeme kila sehemu ili wananchi wapate huduma hiyo.

Kuhusu sekta ya afya alisema Serikali imejipanga kupunguza gharama za matibabu kwa kujenga hospitali kubwa na kuboresha vituo vya afya na Zahanati afya kazi ambayo imeanza kwa kasi na pia itaendelea ikiwa ni malengo ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan anayetaka kuona Watanzania wanapata huduma bora za afya.

Mwisho wake Waziri Mkuu aliwataka wananchi kudumisha amani kama ndiyo tunu ya utuivu wa Taifa la Tanzania.





# SERIKALI YAZIDI KUBORESHA UWEKEZAJI



NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), amesema kuwa Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na ukuaji wa uchumi nchini.

Dkt. Nchemba alisema hayo jijini Dodoma wakati akifungua Mkutano wa Majadiliano ya Kimkakati kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo Ngazi ya Juu, ambao unalenga kubadilishana maarifa, taarifa, na uzoefu kuhusu sera na mikakati ya maendeleo ya nchi.

Alisema Serikali imewasilisha bungeni Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania (Tanzania Investment Act, 2024) na kuanzisha Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi (Tanzania Investment and Special Economic Zones Authority) ili kuboresha mazingira ya uwekezaji.

ìSerikali kupitia Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) na Kituo cha Uwekezaji kati ya Sekta Binafsi na Umma (CPPP) imeendeleza majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika maamuziî, aliongeza Mhe. Dkt. Nchemba.

Mhe. Dkt. Nchemba ambaye ni Mwenyekiti wa Mkutano huo, alisema Serikali pia inaandaa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelezaji wa Uwekezaji (2025/2026 ñ 2034/2035) ambao utakuwa na mpango wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini, unaoeleza majukumu ya kila mdau na viashiria vya kupima maendeleo.

Dkt. Nchemba alibanisha kuwa katika kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi Desemba 2024, Serikali imeongeza uwezo wa uzalishaji umeme kwa asilimia 30.3, hasa kupitia Mradi wa Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) ili kupunguza gharama za biashara.

ìKupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2024, Serikali imepunguza au kuondoa ada na tozo mbalimbali ili kuboresha mazingira ya biasharaî, aliongeza Mhe. Nchemba.

Dkt. Nchemba alisema Serikali pia imepata mafaniko makubwa katika ukuaji wa uchumi jumuishi ambapo idadi ya shule na wanafunzi imeongezeka, vituo vya afya vimeongezeka na huduma zimeboreshwa, huduma za maji zimeongezeka katika maeneo yote nchini pamoja na ongezeko la ajira.

Aidha, alitoa rai kwa wadau wote kushirikiana kwa karibu na Serikali ili kufanikisha utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF) ambao umetilia mkazo utaratibu wa ufadhili wa miradi ya mabadiliko ya tabianchi (climate financing modality) na kuimarisha Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kama njia mbadala za ufadhili.

Kwa upande wake Mwenyekiti Mwenza wa Kundi la Washirika wa Maendeleo na Balozi wa Ireland nchini, Mhe. Nicola Brennan aliishauri Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya biashara kwa kuondoa vikwazo vinavyozuia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni.

Alisema hii itaongeza mchango wa sekta binafsi katika kuleta uwekezaji, ajira, uvumbuzi, na suluhisho kwa changamoto mbalimbali ili kujenga uchumi imara.

ìWadau wa Maendeleo tayari tumekuwa na majadiliano mazuri kuhusu hili, na tunapongeza utayari wa Serikali kushirikiana nasi kuona jinsi bora ya kuondoa vikwazo na kuvutia uwekezaji zaidi wa moja kwa moja wa kigeni (FDI) nchini Tanzania, pamoja na kuimarisha sekta ya biashara ya ndaniî, aliongeza.

Mhe. Brennan alisema Washirika wa Maendeleo watahakikisha kuwa Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050 inapata ufadhili wa uhakika na endelevu, hasa katika sekta za afya, elimu na sekta ya kijamii kwa ujumla.

ìTunapopanga vipaumbele katika matumizi ya rasilimali finyu za Msaada wa Maendeleo (ODA), ni muhimu pia kuelewa vyema vyanzo vingine vya ufadhili vinavyopatikana kwa nchi zenye kipato cha kati nje ya ODA, pamoja na mchango ambao sisi kama Wadau wa Maendeleo tunaweza kutoa kusaidia Tanzania kuzifikia na kuzitumia fursa hizo ipasavyo. Tunatazamia kujadili zaidi suala hili kwa kina.î

Aliahidi kuwa Washirika hao wataendelea kushirikiana na Tanzania kuhakikisha maendeleo yanapatikana na kustawisha jamii.

# CMSA YABAINISHA MAFANIKIO YAKE

NA MWANDISHI WETU

MAMLAKA ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) imesema katika mwaka 2024 kumekuwa na mafanikio makubwa ambayo yamewezesha pia thamani ya uwekezaji katika masoko ya mitaji kuongezeka kwa asilimia 24.7 na kufikia Sh.trilioni 46.7 katika kipindi kilichoishia Desemba 2024, ikilinganishwa na Sh.trilioni 37.4 katika kipindi kilichoishia Desemba 2023.

Pia thamani ya uwekezaji katika hisa za kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa yaani imeongezeka kwa asilimia 22.3 na kufikia Sh.trilioni 17.87 katika kipindi kilichoishia Desemba 2024, ikilinganishwa na Sh.trilioni 14.61 katika kipindi kilichoishia Desemba 2023.

Aidha, thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja imeongezeka kwa asilimia 41.6 na kufikia shilingi trilioni 2.6 katika kipindi kilichoishia Desemba 2024,ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.8 katika kipindi kilichoishia Desemba 2023.

Mafanikio hayo yameelezwa leo Februari 26,2025 jijini Dar es Salaam na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana(CMSA), CPA. Nicodemus Mkama wakati akitoa tathimini yq utendaji wa masoko ya mitaji kwa mwaka 2024.

ìCMSA ina jukumu la kuendeleza na kusimamia masoko ya mitaji hapa nchini, ikiwa ni pamoja na kuwezesha utoaji wa bidhaa mpya na bunifu zinazovutia wawekezaji wa ndani na kimataifa. Katika kutekeleza jukumu hili, katika kipindi cha mwaka 2024, masoko ya mitaji yamepata mafanikio.î

Ametaja baadhi ya mafanikio mengine ambayo yamepatikana ni uwepo wa Bidhaa Mpya na Bunifu ambapo amesema mwaka 2024 umeshuhudia utoaji wa bidhaa mpya na bunifu zinazovutia wawekezaji wa ndani na wa kimataifa.

Amefafanua mathalani, Hatifungani ya kijani ya taasisi ya umma iliyotolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Jiji la Tanga (Tanga-UWASA) kwa ajili ya kutekeleza miradi ya miundombinu ya maji na utunzaji wa mazingira, ambayo ilikusanya Sh.bilioni 54.72, na kuvuka lengo la kukusanya shilingi bilioni 53.2, sawa na mafanikio ya asilimia 103

Vilevile, Hati Fungani ya Miundombinu ya Samia iliyotolewa na Benki ya CRDB ilikusanya Sh.bilioni323.09, kuvuka lengo la kukusanya shilingi bilioni 150,sawa na mafanikio ya asilimia 215.4.

Amesema fedha zilizopatikana zinatarajiwa kuwezesha wakandarasi wa ndani wanaofanya kazi na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA), kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara vijijini na mijini.

Aidha, Hatifungani kwa ajili ya kuendeleza kampuni ndogo na za kati za ujasiriamali (SMEs) iliyotolewa na Benki ya Azania, ambapo kiasi cha Sh.bilioni 63.3kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 210.9.

Pia, Hatifungani aina ya Sukuk iliyotolewa na kampuni ya iTrust Finance, kwa ajili ya kuwekeza katika biashara ndogo na za kati zinazokidhi misingi ya Shariah, ambapo kiasi cha Sh.bilioni 13.27 kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 265. Vile vile, Mauzo ya Hisa Stahiki za Benki ya DCB zenye thamani ya shilingi bilioni 10.74, ambapo mauzo haya yamepata mafanikio ya asilimia 100.

CPA.Mkama pia amesema mwaka 2024, umeshuhudia mwamko mkubwa wa utoaji bidhaa mpya na bunifu katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja, hivyo kuweka wigo mpana wa fursa za uwekezaji kwa watanzania wa kada mbalimbali, ikiwa ni Pamoja na vijana, wanawake na makundi maalumu.

ìCMSA iliidhinisha Mifuko ya Uwekezaji inayoendeshwa na Kampuni ya iTrust Finance Limited, ambapo mifuko mipya mitano ilizinduliwaóiSave, iCash, Imaan, iIncome, na iGrowth.

ìVilevile, Zan Securities na Orbit Securities walizindua mifuko ya Timiza na Inuka, huku Alpha Capital ikianzisha Mfuko wa Halal. Aidha, Sanlam Investments East Africa ilizindua SUTS - SANLAM Unit Trust Scheme, ikijumuisha Sanlam Pesa Money Market Fund na US Dollar Fixed Income Fund.

ìKutokana na juhudi hizi, thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (NAV) iliongezeka kwa asilimia 41.63, kutoka shilingi trilioni 1.84 mwaka 2023 hadi shilingi trilioni 2.61 mwaka 2024. Ukuaji huu umetokana na mikakati ya utoaji wa elimu kwa umma unaofanywa na wadau katika masoko ya mitaji na matumizi ya mifumo ya kidijitali, ambayo imerahisisha upatikanaji wa huduma za masoko ya mitaji mijini na vijijini.îAmesema.

Kuhusu matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano amesema imekuwa na mchango mkubwa katika kuongeza mauzo katika soko la hisa. Matumizi ya teknolojia ya Habari, ikiwa ni pamoja na matumizi ya simu za mkononi yameongeza ushiriki wa wawekezaji wa ndani, hivyo kuongeza ukwasi katika soko la hisa.

Amefafanua katika mwaka 2024, asilimia 24.33 ya mauzo ya hisa yametokana na matumizi ya teknolojia ya habari, ikilinganishwa na asilimia 4.84 mwaka 2023 huku akitoa rai kwa wadau katika masoko ya mitaji kushirikiana na CMSA katika mwaka wa Fedha 2025/2026 kutekeleza mikakati mbalimbali.

Ametaja baadhi ya mikakati hiyo kuongeza juhudi za kutekeleza Mpango Mkakati wa elimu kwa umma kuhusu fursa na faida zinazopatikana kwenye masoko ya mitaji, ikiwa ni pamoja na kutoa machapisho mbalimbali magazetini.

Pia kushiriki kwenye mahojiano ya vipindi vya Redio na Runinga, kutoa semina, warsha na makongamano kwa makundi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na vijana, wanawake na walemavu. Hafla ya leo iliyoandaliwa na Vertex International Securities ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati huo.

Mengine ni kuongeza idadi ya bidhaa, ambapo Mamlaka itaendelea kutoa miongozo ya utoaji na usimamizi wa bidhaa na huduma mpya, bunifu, na zenye mlengo maalum.

Pia Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kutoa huduma za masoko ya mitaji, ambapo CMSA itapitia na kuidhinisha mifumo ya kidigitali inayowezesha ushiriki mkubwa wa wananchi kwenye masoko ya mitaji.

ìHatua hii inatarajiwa kuongeza ushiriki wa wananchi mijini, vijijini katika masoko ya mitaji, na hivyo kuchangia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Tatu wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha.Kwa ujumla, katika kipindi cha mwaka 2024, masoko ya mitaji nchini Tanzania yameimarika na kuonyesha ukuaji mzuri na wa kuridhishaÖ

ìYakichochewa na utoaji wa bidhaa mpya na bunifu, matumizi ya teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Utoaji elimu kwa umma ulioleta mwamko mkubwa kwa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa. Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) itaendelea kutekeleza mikakati yenye lengo la kuchagiza na kujenga uchumi shindani kwa maendeleo ya watu,îamesema CPA.Mkama.



# MAVUNO YA KAHAWA YATIKISA MKOANI RUVUMA

NA MWANDISHI WETU

WAKULIMA wa zao la kahawa wanaohudumiwa na Chama cha Msingi cha Ushirika KImuli Amcos kata ya Utiri Wilaya ya Mbinga Mkoani Ruvuma, wamefanikiwa kuzalisha tani 105,986.95 za kahawa zilizowaingizia zaidi ya Sh.bilioni 14,022,174,698.40 kuanzia Msimu wa kilimo 2021/2022 hadi 2024/2025.

Katibu wa Chama hicho Aron Komba amesema, katika msimu 2021/2022 wakulima walizalisha tani 548,551 zenye thamani ya Sh.bilioni 3,299,453,120,msimu wa kilimo 2022-2023 walizalisha tani 455,643 ambazo ziliwaingizia Sh.bilioni 3,065,405,776.40.

Aidha alisema, msimu wa 2023/2024 Wakulima ambao ni Wanachama wa Kimuli Amcos walizalisha jumla ya kilo 585,288 zenye thamani ya Sh.bilioni 2,929,893,908 na msimu 2024/2025 walizalisha kilo 530,253 ambazo waliuza Sh.bilioni 4,727,421,894 kupitia njia ya minada.

ìPia kwa muda wa miaka minne ya Uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, tumetoa mikopo ya pembejeo yenye thamani ya Sh.bilioni 3,056,783,867 kwa Wakulima 7,005 wanaojishughulisha na kilimo cha kahawa na mazao mengine ya chakula na biasharaîalisema Komba.

Kwa mujibu wa Komba, msimu wa kilimo 2022/2023 wametoa mikopo ya pembejeo ya Sh.957,343,812 kwa wanachama 2,137 mwaka 2023/2024 Sh.917,834,200 kwa Wanachama 2,381 na mwaka 2024/2025 wametoa mikopo yenye thamani ya Sh.1,181,605,855 iliyokwenda kwa Wananchama 2,487.

Alisema, mikopo hiyo imewasaidia Wanachama kulima kwa tija na kuongeza uzalishaji kwani hapo awali walikuwa wanaangaika kutafuta pembejeo ambazo ziliuzwa kwa bei kubwa kati ya Sh.165,000 hadi 170,000 kwa mfuko mmoja wa kilo 25.

Alisema, hali hiyo ilipelekea baadhi ya wakulima kukata tamaa na kutoendelea na shughuli zao za kilimo kutokana na kushindwa kumudu gharama ya pembejeo ambapo, amempongeza Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, kwa kuanza utaratibu wa kutoa pembejeo za ruzuku kwa zao la kahawa.

Komba, ameiomba Serikali kuendelea kutoa pembejeo za ruzuku kwa zao la kahawa ili kuwapunguzia wakulima mzigo mkubwa wa kununua pembejeo kwa bei ya juu na kuongeza upatikanaji wa pembejeo za ruzuku ili wakulima waweze kuzalisha kwa wingi.

ìNaishauri Serikali kama inataka kufanikisha mpango wake wa kutouza kahawa ghafi basi ituwezeshe kwa kutujengea miundombinu ili tuweze kukaanga kahawa tunayozalisha kwa ajili ya matumizi ya sisi wenyewe na watu wengine na nyingine tuuze kwenye soko la nje”alise ma Komba.

***Ametoa ombi kwa Serikali kupitia Wakala wa Barabara za mijini na vijijini(Tarura) Wilaya ya Mbinga, kukamilisha ujenzi wa Barabara ya lami ya Utiri-Mahende kwa kiwango cha lami ili iweze kusaidia wakulima kusafirisha mazao kupeleka sokoni kwa haraka kwani barabara hiyo inapita kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa kahawa.***



Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Amcos ya Kimuli Yordan Komba alisema, katika kipindi cha miaka minne Chama hicho kimepiga hatua kubwa kwa kuongeza Wanachama kutoka 364 tangu kilipoanzishwa mwaka 1993 hadi 1,700 mwaka 2024.

Aidha, ameiomba Serikali kupitia maafisa Ugani kwenda kwa wakulima kuwapa utaalam na mbinu za kilimo cha kisasa zitakazo wasaidia kuongeze uzalishaji na kupata mavuno mengi.

Mkulima na Mwanachama wa Chama hicho Gisat Komba alisema, kwa muda wa miaka minne uzalishaji wa kahawa umeongezeka na hali hiyo imetokana na upatikanaji wa pembejeo za ruzuku zinazotolewa na Serikali ambazo zimehamasisha watu wengi hasa vijana kujikita kwenye kilimo cha zao hilo.

Hata hivyo alisema, changamoto kubwa ni soko la uhakika kwani wanunuzi wana tabia ya kujipangia bei ya kahawa bila kuwashirikisha wakulima jambo linalowaumiza sana kwa sababu wanatumia gharama kubwa katika uzalishaji wake.

Kwa upande wake Afisa Mtendaji wa kata ya Utiri Libaba Gervas Libaba alisema, kata hiyo ni maarufu kwa kilimo cha zao la kahawa na Wananchi wanajitahidi sana kulima, lakini changamoto iliyopo ni upatikanaji wa pembejeo za ruzuku.

Ametoa ombi kwa Serikali kupitia Wakala wa Barabara za mijini na vijijini(Tarura) Wilaya ya Mbinga, kukamilisha ujenzi wa Barabara ya lami ya Utiri-Mahende kwa kiwango cha lami ili iweze kusaidia wakulima kusafirisha mazao kupeleka sokoni kwa haraka kwani barabara hiyo inapita kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa kahawa.

Baadhi ya Wakulima wa zao la Kahawa wa kijiji cha Utiri Wilaya ya Mbinga Mkoani Ruvuma wakiangalia uzalisha kwenye miche ya kahawa katika moja ya shamba linalomilikiwa na Chama cha Msingi cha Ushirika Kimuli Amcos.



# MSAADA WAKISHERIA WA DK SAMIA WAPONGEZWA



NA MWANDISHI WETU

MKUU wa Wilaya ya Longido, Salum Kalli amesifu juhudi za wizara ya Katiba na Sheria kwa kuwaletea wananchi huduma ya msaada wa kisheria bure na kusisitiza kuwa wananchi wa Arusha wanapaswa kuitumia ipasavyo kwa manufaa yao na jamii kwa ujumla.

Pia amewataka wakazi wa mkoa wa Arusha kuchangamkia fursa ya kipekee ya kupata msaada wa kisheria kupitia Mama Samia Legal Aid Campaign inayoendelea jijini Arusha.

Akizungumza Juzi, alipotembelea mabanda ya huduma za kisheria katika viwanja vya TBA jijini Arusha, Kalli amesema kuwa kampeni hiyo itadumu kuanzia Machi 1 hadi Machi 8, 2025 na ni nafasi muhimu kwa kila mwananchi mwenye changamoto za kisheria kufika na kupata msaada bure.

ìHii ni fursa adhimu kwa kila mwenye changamoto za kisheria. Kuanzia masuala ya mirathi, migogoro ya ardhi, ndoa, na mengineyo. Napenda kuwaalika wananchi wote, hususan wanawake wanaokabiliwa na changamoto hizi, kufika na kupata msaada wa kisheria bila malipo,î amesema Kalli.

Aidha, ametoa mfano wa mama mjane ambaye amenyangíanywa mali alizochuma na mume wake baada ya kufariki. Kupitia kampeni hii, mama huyo na wengine wenye changamoto kama hizo wanaweza kupata haki zao kwa msaada wa wataalam wa sheria waliopo kwenye mabanda hayo.

ìHii ni kampeni muhimu inayohakikisha haki inapatikana kwa wote, hususan wale waliokosa sauti ya kutetea haki zao,î ameongeza.

Mama Samia Legal Aid Campaign inaendelea jijini Arusha hadi Machi 8, 2025, ikiwa na lengo la kuwasaidia wananchi kupata haki zao bila gharama yoyote.

Wakati msaada huo ukiendelea kupokewa kwa matumaini sehemu mbalimbali nchini hivi karibuni Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini, amewataka wananchi kutoa maelezo sahihi kwa watoa huduma za msaada wa kisheria ili kufanikisha kutatua changamoto zinazowakumba, na kuhakikisha kuwa migogoro ya ardhi, mirathi, ndoa na masuala mengine ya kisheria yanapata ufumbuzi kwa wakati.

Sagini ameyasema hayo leo mkoani Arusha wakati alipotembelea banda la Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na mabanda mengine kuelekea wiki ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambayo itafanyika Machi 8 mwaka huu mkoani Arusha.

Aidha maadhimisho hayo ambayo yanatangulizwa na maonyesho kutoka kwa taasisi na mashirika mbalimbali, amewataka wananchi kutumia fursa hiyo kufika kwa wingi katika mabanda hayo kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali za kisheria sambamba na kutatuliwa kero za zinazowakabili kwa wakati.

Aidha Sagini amekazia umuhimu wa kampeni ya Mama Samia Legal Aid inayolenga kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi wenye changamoto za kisheria.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda ameagiza watoa huduma za msaada wa kisheria kwenye kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa kisheria ya Mama Samia, kuhakikisha kuwa wananchi wote waliofika kupata msaada wa kisheria wanasikilizwa na kutatuliwa changamoto zao kikamilifu.

Makonda amesema kuwa ,lengo la wananchi kufika kwenye mabanda hayo ni ili kupata haki zao za msingi kwa wakati na kutatuliwa kero zao kupitia kampeni ya Samia Legal Aid inayotolewa viwanja vya TBA.

Makonda amesema wananchi wanaofika katika banda hilo wanatakiwa kusikilizwa na kuhudumiwa ili waweze kutoa malalamiko yao ikiwemo kuangalia kwa makini changamoto zao hususani katika idara ya kazi, sheria, haki za watoto na mengineyo.

Aidha Makonda ametumia fursa hiyo pia kuwasihi wananchi wa mkoa wa Arusha kujitokeza kwa wingi kupatiwa msaada huo wa kisheria ili migogoro yao iweze kutatuliwa kupitia uwezeshaji uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan uliotokana na wazo lake hili la kuwa na kampeni ya kitaifa ili kuwafikia wananchi wanyonge na wale wanaokosa haki zao kulingana na sheria.

Nao baadhi ya wananchi waliofika kupata huduma kwenye banda hilo wamesema kuwa, wanashukuru serikali kwa kuwasogezea huduma karibu ili waweze kutatuliwa changamoto zao na kuweza kupata elimu zaidi kuhusu maswala ya kisheria ambayo yamekuwa ni changamoto kwa wengi wao kutokana na kutozijua sheria mbalimbali .


ìKwa kweli tunashukuru sana kwa jambo hili kwani limetupa fursa kubwa sisi kuweza kujifunza na hata kutatuliwa changamoto zetu ambazo zilikuwa zimedumu kwa muda mrefu na kuweza kupata huduma hiyo bure pia tunamshukuru sana Rais Samia kwa kuanzisha hii kampeni ambayo inalenga kutatua changamoto mbalimbali za mambo ya kisheria.îamesema.

# Michezo Kimataifa

## Tetesi za soka



CHELSEA wanaamini wanaweza kufanya dili kwa ajili ya mlinzi wa Sporting Ousmane Diomande msimu wa joto - chini ya kipengele cha ukubwa wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 21. (TeamTalk),



JUVENTUS wameipa Chelsea ruksa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal, hii imetokana na mazungumzo mazuri kati ya klabu hizo na pia maslahi yaliyoridhiwa na pande hizi mbili.




1

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Vinicius Jr, atakuwa na fursa ya kuhamia ligi kuu ya Saudi Arabia kwa pauni milioni 200 msimu wa joto, wakati atakapokuwa imesalia miaka miwili kwenye mkataba wake na Real Madrid. (Telegraph)

BAADA ya kulaulimiwa kwa muda mrefu kuwa tatizo la Arsenal ni kudharau kufaya usajili hasa eneo la ufungaji, hatimaye klabu hiyo imesikia kilio hicho na sasa imeanza mawindo makali ili kutibu pengo lililopo, kufutia mkakati huyo klabu hiyo imeingia chimbo na kumnasa Straika makali Raia Slovenia anayekipiga katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani





## TFF YABARIKI ULIPAJI KODI NCHINI

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania-TFF, Bw. Wallace Karia, amekubali mapendekezo ya Serikali na kuahidi kuwa suala la ulipaji kodi ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa. Aidha ameahidi kuwa watalichukulia kwa uzito suala la Kodi katika michezo yote ya mpira wa miguu inayosimamia na Taasisi hiyo.

Kauli hiyo imetolewa katika kikao cha majadiliano kati yake na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Na (Mb) na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Profesa Palamagamba Kabudi. Kikao hicho pamoja na masuala ya kodi walijadili maendeleo na changamoto zinazoikabili sekta ya michezo hususan mpira wa miguu nchini. Katika mazungumzo hayo yaliyofanyika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam, Serikali imeipongeza TFF na Bodi yake ya Ligi, kwa kusimamia kwa weledi masuala ya maendeleo ya soka na kuliletea Taifa heshima kubwa barani Afrika kiasi cha kupewa jukumu la kuandaa mashindano ya CHAN na AFCON. Pia serikali ilikubaliana na namna tasnia ya utamaduni, sanaa na michezo inavyoweza kutumika kuhamasisha uzalendo wa kulipa kodi kwa hiari, kupitia kampeni ya kudai na kutoa risiti kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Majadiliano hayo yaliwashirikisha viongozi wa juu wa Wizara ya Fedha, akiwemo Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya, Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA, Bw.Yusuph Mwenda, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania- TFF, Bw. Wallace Karia, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Bw.. Almas Kasongo, viongozi waandamizi wa Wizara ya Fedha, pamoja na Taasisi zinazosimamia michezo nchini.



# SIKIA KISA CHA TALAKA INAYOSISIMUA - 1

NA MWANDISHI WETU

MAHUSIANO ya kimapenzi ya Mfalme wa jamii ya Wazulu kutoka Afrika Kusini yamezua mjadala nchini humo, huku gumzo linalohusiana na maisha yake ya kibinafsi likisambaa kwa kasi kama moto wa nyikani katika jamii hiyo ambayo inakumatia utamaduni wake. Mfalme wa Zulu anasemakana kuvunja kanuni za kitamaduni kwa kutaka kutoa talaka, jambo ambalo haliendani na itikadi za jamii hiyo.

Mume kuwa na wake wengi ni mojawapo ya masuala yanayokubalika katika jamii ya Wazulu, lakini Mfalme Misuzulu kaZwelithini amefanya uamuzi ambao sio wa kawaida kwa kuwasilisha kesi mahakamani ya kutaka kumtalaki mke wake wa kwanza, Malkia Ntokozo kaMayisela.

"Kila mmoja ameshangazwa. Watu hawakutarajia kwamba yangefikia kiwango cha kutaka kuotoa talaka,' alisema Profesa Gugu Mazibuko ambaye ni mtaalamu wa utamaduni katika chuo kikuu cha Johannesburg huko Afrika Kusini.

'Katika utamaduni wa jamii ya Wazulu, hakuna talaka. Haupaswi kumfukuza mke wako,' alisema.

Mfalme wa Jamii ya Wazulu anayefahamika kama 'Simba wa taifa,' ndiye mwenye kuhifadhi tamaduni za jamii hii ambazo ni za jadi. Tamaduni hizi zimedumisha ndoa na husiana ndoa ya wake wengi kama jambo kubwa kabisa la mafanikio ya ufalme.

Na japo majukumu yake nchini Afrika Kusini ni ya kitamaduni na hayana uzito katika sheria za nchi hiyo, kiongozi huyu wa jamii anasalia kuwa na ushawishi mkubwa katika jamii huku ofisi yake ikipokea ufadhili wa mamilioni ya dola za Kimarekani kutoka kwa serikali kuu.

Mfalme huyo ambaye alikulia katika taifa jirani la Eswatini , alipata masomo yake nchini Marekani na kukabidhiwa wadhifa wa uongozi mnamo 2021. Aidha amekuwa akikabiliwa na utata tangu awali.

Kukabidhiwa kwake mamlaka kulipingwa mahakamani na kaka yake mkubwa ñ ambaye ni wa mama mwingine ñ aliyetaka kupokezwa ufalme huo.

Ndoa yake ya pili, imegonga vichwa vya habari, na jaribio lake kuoa mke wa tatu limegongwa mwamba huku kukiwa na ripoti kwamba ana uhusiano kwa kando na mwanamfamle wa kike.

Hata hivyo, kashfa inayozunguka maisha ya kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 50 imekuwa ikijadiliwa chini kwa chini ñ hadi pale alipotangaza azma ya kumtalaki mke wake na kuwasilisha ombi rasmi mahakamani mwezi Desemba.

Profesa Madibuko amekiri kwamba kumbukumbu za historia ya Wa Zulu zinaonyesha kwamba kuna mfalme ambaye katiak karne ya 20 alimtalaki mmoja wa wake zake , ' ila hilo lilifanyika kimya kimya na kuwa siri kubwa katika familia hiyo ya kifalme,' ikizingatiwa kwamba talaka katika ufamle wa zulu sio jambo la kawaida.

'Ikiwa uhusiano utavunjika, basi mke huyu ataendelea kuishi katika boma la mfalme. Atapewa eneo lake kando, na hatakuwa na uhusiano an mfalme , ila yeye na watoto wake watatunzwa.'

Mama Myeni na Mfalme Misuzulu KaZwelithini. Chanzo cha picha,KwaZulu-Natal

Maelezo ya picha,Mfamle huenda ameahirisha ndoa yake ya mke wa tatu Nomzamo Myeni, ila wapenzi hao walionekana pamoja katika hafla ya kitaifa.

Ilikuwa muda kabla ya kupokezwa ufalme ñ punde tu baada ya kifo cha ghafla cha baba na mama yake miaka minne iliyopita ñ kwamba mwanamfalme (wakati huo) Misuzulu alipomuoa Ntokoto Mayisela.

Wawili hao walikuwa tayari kwenye uhusiano wa kimapnenzi na walikuwa tayari ni wazazi wa Watoto wawili , ila kwa mujibu wa mtaalamu mwingine wa utamaduni wa jamii ya Zulu, Prof Muza Xulu kutoka chuo kikuu cha Zululand, uamuzi wa kufunga ndoa ulionekana kuharakishwa.

'Ilionekana kwamba mwanafalme hangeweza kuwa mfalme ikiwa hakuw ana mke,' alioambia BBC.

Malkia kaMayisela alitokea familia ya kawaida ñ kama wake wengine wa wafalme wa Kizulu ñ kutoka mji mdogo wa uchimbaji madini katika jimbo la KwaZulu ñ Natal.

'Malkia alimvutia Mfalme katika mgahawa mmoja kwenye mji wa pwani wa Durban alipokuwa akifanya kazi kama muimbaji,'alisema Prof Xulu.

Hadhi yake katika familia iliwekwa wazi wakati wa kutawazwa kwa mfalme mnamo Desemba 2022 alipoketi kando yake.

Ila nafasi yake sasa inatishika , anapotaja Mume wake kwamba wawili hao hawajaishi pamoja kama mume na mke kwa mwaka mmoja uliopita na kwamba ndoa yao imevunjika.

Kasri ya mfalme ilifuatilizia matamshi yake kwa kutuma mualiko wa ndoa ya Mfamle kwa mke mwingine, Nomzamo Mayeni mwishoni mwa mwezi Januari . Mahari ya bibi harusi inayofahamika kama LOBOLA kwa lugha ya kizulu imeshalipwa ñ huku ng'mbe wanaothaminiwa sana katika jamii hiyo wakitolewa kama mahari.

Malkia kaMayisela hajapokea haya yote vyema, akitaja kwamba huenda akawasilisha malalamishi ya kutaka ndoa hiyo kutofanyika , hali iliyosababisha ndoa hiyo kuahirishwa.

Ameiambia mahakama kwamba , mfalme ambaye anatambulika miongoni mwa jamii hiyo kama "ingonyama", kumaanisha simba, angekuwa anavunja sheria za ndoa kwa kufunga ndoa ya pili japo mke wa kwanza yupo. Anasema pia kwamba hatua hiyo inafanyika chini ya ndoa iliyofanyika katika ofisi ya mwanasheria mkuu ambayo haikubaliwi kuwa na wake wengi na kwamba kabla

>> Itaendelea toleo lijalo...



JAMVI LA HABARI
SPOTI
JUMANNE MACHI 04, 2025



## Master J amuomba Alikiba Msamaha

>> Soma Uk. 15

# MPANZU APEWA JINA JIPYA KUIUA YANGA




NA MWANDISHI WETU

SIKU zinazidi kukimbia kuelelekea mchezo wa soka wa kihistoria nchini, utakaozikutanisha timu kongwe Yanga na Simba zitakazogombea Pointi tatu kila moja, ukiwa ni mzunguko wa pili wa Ligi Kuu ya NBC.

Klabu hizo kongwe Yanga ilianzishwa mwaka 1935 kisha Simba ikafuata mwaka mmoja baadaye 1936 huwa hazina mechi ya kirafiki, kila zinapokutana ni vita kuu kuanzia mashabiki mpaka wachezaji wenyewe ndani ya uwanja.

Safari hii timu hizo zinakutana zikiwa katika wakati muhimu kwa kila moja ikitaka kushinda ili ijiweke vizuri katika msimamo wa ligi.

Ifahamike kwamba Yanga wanautaka zaidi mchezo huo kwa vile ushindi wa Jumamosi hiyo ya Machi 8, utaihakikishia nafasi ya kutetea ubingwa wake iliyoutwaa kwa misimu mitatu sasa.

Endapo itapoteza mchezo huo huenda kauli ya watani wao wa jadi Simba itakuwa inaanza kutimia, kwani mwanzoni tu mwa michuano hii ilitangaza vita rasmi ya kurejesha ubingwa wake katika mtaa wa Msimbazi.

Katika kuongeza vikombowezo kama ilivyo ada inapokaribia mchezo wa aina hiyo, safari hii Simba imempa jina jipya mchezaji wake wa nafasi ya kiungo mshambuliaji Raia wa DRC Elie Mpanzu.

## Macho ya wananchi kwa Azizi Ki Jumamosi

NA MWANDISHI WETU

MASHABIKI wa Yanga kama ilivyo kwa wenzao wa Simba wanachotamani ni kuona timu yao inashinda tu dhidi ya Simba na siyo vingine, lakini kazi hiyo licha ya kufanywa na wachezaji mbalimbali ndani ya kikosi cha Wananchi hao, lakini macho mengi zaidi yameelekezwa kwa 'Bwana harusi' Aziz Ki.

Staa huyo ndani ya kikosi cha Yanga hivi karibuni alidumu midomoni mwa mashabiki na wapenda burudani kwa ujumla, pale alipofunga ndoa ya kifahari na msanii maarufu Tanzania




Hamisa Mobeto. Muda mfupi baada ya kufanyika tukio hilo lililokusanya idadi kubwa ya mastaa Jijini Dar, mashabiki wa timu hiyo na hata wapinzani wao walianzisha minong'ono wakidai huenda kiwango cha mwamba huyo uwanjani kinaweza kupungua kutokana na matumizi ya ndoa yaliyomkabili kwa zaidi ya wiki nzima.

Lakini tofauti na matazamio hayo mwamba huyo akawa ndiyo kama amezidisha moto, kwani alikuwa akipachika mabao na kutoa asisti katika mechi mbalimbali zilizofuata na kuisaidia timu yeke kudumu kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu ikifikisha Pointi 58.



## Man U, Man City ndani ya chungu kimoja

**WABABE WA** Soka la Jijini la London Manchester United wamejikutya wakitamani sehemu inayofikiriwa na watani zao wa jadi Manchester City wakimwania winga machachari Raia...

>> Inaendelea Uk. 14

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM